

**KIZIDUO CHA MKUTANO WA BARAZA LA MADIWANI LA KAWAIDA
LILILOFANYIKA TAREHE 28/07/2017, KATIKA UKUMBI WA
HALMASHAURI YA WILAYA YA RUNGWE WA JOHN A. MWANKENJA**

Katika mwaka wa fedha 2016/2017, Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe ilifanikiwa kufanya mikutano ya kawaida minne kama ilivyopangwa katika ratiba ya vikao vya Halmashauri. Vilevile, katika mikutano hiyo maazimio mbalimbali yalitolewa na kuagiza Menejimenti kutekeleza maagizo hayo, maagizo hayo ni kama ifuatavyo:-

- (i) Waheshimiwa Madiwani pamoja na watalaam washirikiane katika kudhibiti utorohaji wa mapato ya Halmashauri ambapo itasaidia kuongeza mapato ya Halmashauri.
- (ii) Mkurugenzi Mtendaji Wilaya awasimamie vizuri Watendaji wa Kata na Watendaji wa Vijiji ambao ni wahusika katika ukusanyaji wa mapato katika maeneo yao.
- (iii) Kuliridhiwa ombi la ununuzi wa mitambo ya matengenezo ya barabara kwa mkopo wa Tshs.1,338,120,000.00 kutoka kwenye taasisi ya fedha ya TIB
- (iv) Kulipitishwa Sheria Ndogo ya Kodi ya Majengo ya Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe za mwaka 2016.
- (v) Kuboreshwe kamati za mapambano ya kudhibiti maambukizi ya UKIMWI kwenye Kata.
- (vi) KAMAKA zisimamie WMAC ili kufanya kazi kwa ufanisi katika maeneo yao.
- (vii) Kuendelea kutolewa huduma ya tohara katika Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe ikiwa ni pamoja na kuendelea kutoa elimu katika jamii kutumia kinga ili kupambana na maambukizi ya VVU/UKIMWI. Pia kondomu zisambazwe maeneo mbalimbali kama ilivyokuwa inafanyika awali (miaka ya nyuma).
- (viii) Kufanyike maboresho ya daftari la wapiga kura katika Kata ya Ibigi ili makosa yasijirudie ya watoto walio chini ya miaka 18 walioandikishwa kupiga kura tena katika uchaguzi wa marudio.
- (ix) Watendaji wa Kata kukumbushwa kwa barua kuwa wanatakiwa kuwasimamia ipasavyo watumishi wote walioko kwenye Kata zao
- (x) Kufanyike mchakato wa Mamlaka ya Mji Mdogo wa Tukuyu kuwa Mamlaka Kamili.
- (xi) Kuchukuliwe hatua kwa Watendaji wa Kata ambao makusanyo ya mapato yapo chini kwa mwaka wa fedha 2016/2017, na Watendaji wa Kata waliokusanya vizuri wapewe pongezi.
- (xii) Watendaji wa Kata na Vijiji wajulishwe kuwa wanatakiwa kukaa kwenye vituo vyao vya kazi.

- (xiii) Taarifa za mapato ya Kata kila robo kwa mwaka wa fedha 2016/2017, ipelekwe kwenye Kata zote za Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe.
- (xiv) Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango itoke kwenda kukagua vyanzo vya mapato katika Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe, ikiwa ni pamoja na kuangalia namna mapato yanavyokusanywa na kutoa ushauri kwenye changamoto katika ukusanyaji wa mapato ili kuboresha mapato ya ndani.
- (xv) Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe iendelee kutenga fedha asilimia 10 (10%) kwa ajili ya kupeleka kwenye vikundi vya wanawake na vijana.
- (xvi) Halmashauri ihakikishe inasimamia ipasavyo mkataba mpya utakaowekwa kati ya Kitongoji cha Ikama na Kampuni ya TOL gesi kwa ajili ya manufaa ya wananchi na Halmashauri kwa ujumla.
- (xvii) Idara ya Maji iendelee kusimamia ipasavyo miradi ya maji ili wananchi waweze kupata huduma hiyo kiurahisi na kwa wakati.
- (xviii) Halmashauri ilipe madai ya Walimu wa shule za msingi waliohamishwa kupelekwa kwenye shule mbalimbali katika Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe.
- (xix) Kamati ya Uchumi, Ujenzi na Mazingira iendelee kulifanyia kazi suala la mgogoro uliopo katika kiwanda cha maziwa cha Katabe.
- (xx) Kamati ya Uchumi, Ujenzi na Mazingira iendelee kulishughulikia suala la gharama za upimaji wa ardhi ili gharama hizo ziendane na kipato cha wananchi wa Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe.
- (xxi) Mkutano ulipokea na kuipitisha taarifa ya watumishi waliokuwa na vyeti feki.
- (xxii) Kulitolewa maamuzi mbalimbali katika taarifa ya utekelezaji wa masuala ya nidhamu ya watumishi kwa kipindi cha Januari hadi Machi 2017.
- (xxiii) Kulipokelewa na kuridhiwa taarifa ya uteuzi wa Wakuu wa Idara baada ya upekuzi kukamilika.
- (xxiv) Kuliidhinishwa mapendekezo ya uteuzi wa Wakuu wa Idara.
- (xxv) Kuliidhinishwa mapendekezo ya kuthibitisha kazini Mkuu wa Idara kwa mwaka 2017.
- (xxvi) Halmashauri kutekeleza agizo la kutenganisha Ofisi za Serikali na ofisi za vyama vya Siasa kwenye maeneo ya ofisi za Kata au Vijiji.



.....
MHE: EZEKILE MWAKOTA

MWENYEKITI



.....
BIBI: LOEMA I. PETER.

KATIBU